# *Mwongozo wa Kamati ya Uandikishaji na Ukaguzi wa Elimu ya Umma Inayofaa ya Bure na Elimu ya Mafunzo ya Ziada*

Aprili 15, 2021

Idara ya Elimu ya Kentucky
(Kentucky Department of Education)

*Ufuatao ni mwongozo usio na udhibiti ulioundwa kutumika kwa kushirikiana na ulinzi wa utaratibu kwa wanafunzi wenye ulemavu chini ya Sheria ya Elimu ya Watu wenye Ulemavu (Individuals with Disabilities Education Act (IDEA)). Mwongozo husahihishwa kulingana na maoni ambayo Ofisi ya Elimu Maalum na Mafundisho ya Mapema (Office of Special Education and Early Learning (OSEEL)) hupokea kutoka kwa wakurugenzi wa Elimu Maalum, vikundi vya washikadau wa jimbo, jinsi sheria ya Idara ya Elimu ya Kentucky (Kentucky Department of Education's (KDE)) inavyosema, kesi za korti na mwongozo kutoka kwa Ofisi ya Mpango wa Elimu Maalum (Office of Special Education Programs (OSEP)). OSEEL pia husahihisha mwongozo kulingana na ziara za ufuatiliaji wa eneo, ukaguzi wa dawati na malalamiko rasmi yaliyoandikwa.*

# Jedwali la Yaliyomo

Kusudi ........ 3
Elimu ya Umma Inayofaa ya Bure (Free Appropriate Public Education (FAPE)) ........ 3
Je, Elimu ya Mafunzo ya Ziada ni nini? ........ 3
Jukumu la ARC ........ 4
Maoni ya Mzazi ........ 4
Kuamua Ustahiki wa Elimu ya Mafunzo ya Ziada ........ 5
Kuamua Dakika za Huduma ya Elimu ya Mafunzo ya Ziada ........ 7
Jinsi ya Kuandika Maamuzi ya Elimu ya Mafunzo ya Ziada ........ 7
Kupanga Mikutano ya ARC ........ 7
Kupanga Huduma za Elimu ya Mafunzo ya Ziada ........ 8
Watoa Huduma wa Nje ........ 8
Usafiri ........ 8
Mahudhurio ........ 9
Mazingatio ya Kifedha ........ 9
Idadi ya Wanafunzi ........ 9
Fursa za Shule Nzima ........ 9
Kuandika Huduma za Elimu ya Mafunzo ya Ziada ........ 10
Mambo Muhimu ya Kukumbuka ........ 10
Rasilimali za ARC ........ 11
Maswali Yaliyopendekezwa ya Kuongoza ARC kuhusu Elimu ya Mafunzo ya Ziada ........ 12
Mfano wa Kumbukumbu ya Elimu ya Mafunzo ya Ziada ........ 13
Rasilimali kwa Wazazi na Familia ........ 14
Mwongozo wa Mzazi na Familia kwa Mifano ya Utoaji wa Mafundisho na Elimu ya Umma Inayofaa ya Buree ........ 15
Mwongozo wa Mzazi na Familia kwa Elimu ya Mafunzo ya Ziada ........ 18

**Kusudi**

Mwongozo huu unakusudiwa kusaidia Kamati ya Uandikishaji na Ukaguzi (Admissions and Release Committee (ARC)) kufanya maamuzi ya mtu binafsi kuhusu utoaji wa huduma za elimu ya mafunzo ya ziada.

**Elimu ya Umma Inayofaa ya Bure (Free Appropriate Public Education (FAPE))**

*Kanuni za Usimamizi za Kentucky* zinafafanua elimu ya umma inayofaa, ya bure (FAPE) kama "elimu maalum na huduma zinazohusiana ambazo:

(a) Hutolewa kwa gharama za umma, chini ya usimamizi na maelekezo ya umma, na bila malipo;

(b) Hufikia viwango vya Idara ya Elimu ya Kentucky iliyojumuishwa katika 707 KAR Sura ya 1 na Mpango wa Masomo, 704 KAR 3:303, kama inavyofaa;

(c) Hujumuisha shule ya chekechea, shule ya msingi, au elimu ya shule ya sekondari katika jimbo; na

(d) Hutolewa kwa mujibu wa mpango wa elimu ya mtu binafsi ( individual education program (IEP)) ambao unakidhi mahitaji ya 707 KAR 1:320."

Katika hatua za mwanzo za janga la COVID-19, wilaya za shule za eneo husika zilibadilika haraka na kuanza kutumia Mafundisho Yasiyo ya Kawaida (Non-Traditional Instruction (NTI)) kama njia ya kuwaweka wafanyakazi na wanafunzi salama. Katika kipindi chote cha janga la COVID-19, wilaya za eneo husika zimetoa mifano mbalimbali ya mafundisho ikiwa ni pamoja na mafundisho ya kikundi kidogo, ya ana kwa ana, NTI, au ya mseto inayojumuisha ana kwa ana na NTI.

Bila kujali njia ya utoaji wa mafundisho, wilaya za shule za eneo husika zinaendelea kuwa na jukumu la kutoa FAPE kwa wanafunzi wenye ulemavu.

Wakati wowote ambapo elimu maalum na huduma zinazohusiana hazitolewi kulingana na Mpango wa Elimu ya Mtu Binafsi (IEP), bila kujali sababu, hii inaweza kusababisha madai ya kukataliwa kwa FAPE. Suluhisho pekee la kushindwa kutoa FAPE ni huduma za elimu za fidia.

**Je, Elimu ya Mafunzo ya Ziada ni nini?**

Ingawa elimu ya mafunoz ya zaiada haijafafanuliwa katika Sheria ya Elimu ya Watu Wenye Ulemavu (Individuals with Disabilities Education Act (IDEA)) au *Kanuni za Usimamizi za Kentucky*, ufafanuzi huo umeundwa na sheria ya kesi na mwongozo usio wa udhibiti kutoka kwa Ofisi ya Mipango ya Elimu Maalum (Special Education Programs (OSEP)) ya Idara ya Elimu ya Marekani (United States Department of Education's (USED)).

Elimu ya mafuno ya ziada imeundwa ili kulinda haki ya wanafunzi wenye ulemavu kwa FAPE. Kusudi la elimu ya mafunzo ya ziada ni "kulenga kuwaweka watoto walemavu katika nafasi ile ambayo wangechukua lakini ikiwa wilaya ya shule haingekiuka IDEA" (*Reid v. Dist. of Columbia*, 43 IDELR 32 (DC Cir. 2005)).

Kuna wakati ambapo wilaya haziwezi kutoa FAPE kwa wanafunzi wote kwa sababu zisizoweza kuepukika. Mfano wa nyakati kama hizo ni wakati wa mwanzo wa janga la COVID-19 wakati shule hazikuweza kutoa mafundisho ya ana kwa ana na huduma zinazohusiana kwa sababu ya tishio kwa afya ya umma.

Huduma nyingine za IEP zilikuwa haziwezi kutekelezwa kupitia NTI, na kusababisha kushindwa kutekeleza IEP kama ilivyoandikwa. Hatimaye, huenda hii ilisababisha kukataliwa kwa FAPE bila kosa la wilaya. Hata hivyo, bila kujali sababu, suluhisho pekee la tatizo la kushindwa kutoa FAPE ni kutoa elimu ya mafunzo ya ziada.

Jumuiya ya elimu imekuwa ikijadiliana kwamba kutumia neno "elimu ya mafunzo ya ziada" kunaashiria kuwa wilaya za eneo husika zinalaumiwa kwa kufanya kitu kibaya, na hivyo kunaweza kuhatarisha uhusiano na familia. Kutokana na jambo hilo, maneno mbadala yameanza kutumiwa kama njia za kujadili huduma zilizoathiriwa na janga la COVID-19 bila kutumia neno "elimu ya mafunzo ya ziada." Maneno kama vile "mafundisho ambayo hayajakamilika," "kukosa mafundisho" na "mafundisho ya baada ya COVID" yanatumika kama maneno mbadala ya "elimu ya mafunzo ya ziada" katika muktadha huu.

Ingawa OSEEL huzuia wilaya kuepuka kutumia neno "elimu ya mafunzo ya ziada," baadhi ya wafanyakazi wa wilaya wanaweza kuona kwamba ni rahisi kutumia lugha mbadala wakati wa mazungumzo haya. Wilaya zinapaswa kujadili na wakili wao wa bodi ya eneo husika kuhusu ikiwa kuna neno linalopendelewa katika muktadha huu.

Haijalishi jina ambalo wilaya itaamua kuita huduma hizo, ikiwa zinakusudiwa kumsaidia mwanafunzi kufidia nafasi za kujifunza au zilizopotea kwa sababu mwanafunzi alinyimwa huduma za FAPE, basi huduma hizo huchukuliwa kuwa elimu ya mafunzo ya ziada.

## Jukumu la ARC

ARCs zinafafanuliwa na 707 KAR 1:002, Kifungu cha 1 (1) kama kikundi cha watu binafsi "wanawajibika katika kutengeneza, kukagua, au kurekebisha mpango wa elimu ya mtu binafsi (individual education program (IEP)) kwa ajili ya mtoto mwenye ulemavu." Watu wanaoweza kuwa wanachama wa ARC ni pamoja na wazazi wa mwanafunzi, mwalimu wa elimu ya kawaida wa mwanafunzi, mwalimu wa elimu maalum anayejua mwanafunzi au ulemavu, mwakilishi wa wilaya, pamoja na wafanyakazi wa huduma zinazohusiana na mwanafunzi inapofaa.

ARCs lazima zikague hali ya elimu maalum na huduma zinazohusiana na ufuatiliaji wa maendeleo unaoendelea kwa kuzingatia kila kesi ili kufanya maamuzi yaliyobinafsishwa kuhusu ikiwa, na kwa kiwango gani, elimu ya mafunzo ya ziada inadaiwa. ARC ikiamua kuwa huduma za elimu ya mafunzo ya ziada zinahitajika, ARC lazima pia ieleze aina, eneo na kiasi cha huduma zitakazotolewa.

## Maoni ya Mzazi

Wazazi ni wanachama muhimu wa ARC. Kanuni za 707 KAR 1:320, Kifungu cha 4 (1) zinahitaji wilaya zihakikishe kuwa mzazi mmoja au wote wawili wa mwanafunzi mwenye ulemavu wanahudhuria kila mkutano wa ARC au wanapewa fursa ya kushiriki.

Maoni ya wazazi na uamuzi wa kitaalamu ni muhimu wakati wa kuamua muda wa mikutano ya ARC ili kujadili elimu ya mafunzo ya ziada. Mzazi akiomba mkutano wa kujadili elimu ya mafunzo ya ziada, wilaya zinapaswa kujibu haraka kwa kupanga mkutano wa ARC. Wakati wa kuwaalika wazazi kwenye mikutano ya ARC, wilaya zinapaswa kubainisha kuwa elimu ya mafunzo ya itajadiliwa katika mkutano. Zinaweza kufanya hivyo kwa kutia alama kwenye kisanduku cha *Nyingine* kwenye Notisi ya Mkutano wa ARC na kuandika "kujadili elimu ya mafunzo ya ziada."

Ili kuwezesha ushiriki wa maana wa wazazi katika mikutano ya ARC, wilaya zinapaswa kuzingatia kuelezea elimu ya mafunzo ya ziada kwa maneno wazi na rahisi mwanzoni mwa mkutano kwani wazazi wengi hawana ujuzi maalum katika nyanja ya elimu maalum. Hii inapaswa kutokea kabla ya kujadili data yoyote ya kiwango cha mwanafunzi na itawapa wazazi fursa ya kuelewa data itakayojadiliwa na jinsi maamuzi kuhusu elimu ya fidia yatakavyofanywa kabla ya kushiriki katika mazungumzo kuhusu watoto wao.

*Mwongozo wa Mzazi na Familia wa Elimu ya Mafunzo ya Ziada* unaweza kutumika kusaidia ushiriki wa wazazi katika kuamua ikiwa kukataliwa kwa FAPE kulitokea na aina za huduma za elimu ya mafunzo ya ziada zinazoweza kuhitajika kumsaidia mwanafunzi katika hali hiyo.

Wazazi lazima wapewe fursa ya kusema wasiwasi wao na kutoa taarifa kuhusu majibu ya mtoto wao kuhusu NTI.

*Mwongozo wa Mzazi na Familia wa Mifano ya Utoaji wa Mafundisho na Elimu ya Umma Inayofaa ya Bure (FAPE)* inaweza pia kusaidia katika majadiliano kuhusu FAPE.

## Kuamua Ustahiki wa Elimu ya Mafunzo ya Ziada

Ili mwanafunzi astahiki kupata elimu ya mafunzo ya ziada, lazima awe alinyimwa FAPE. ARC itafanya uamuzi wa mtu binafsi ili kujua ikiwa alinyimwa FAPE na ikiwa ndivyo, basi huduma gani za elimu za mafunzo ya ziada zinazohitajika.

Kuwa na ujuzi na uzoefu wa kesi za Mahakama Kuu ya Marekani*Hendrick Hudson v. Rowley*[1] na *Endrew F. v. Douglas County*[2] kutasaidia ARC kuamua ikiwa alinyimwa FAPE. Kuanzia na kesi ya *Deal dhidi ya Hamilton*[3] katika Mzunguko wa 6, kiwango cha FAPE kiliwekwa ili kutoa "mafao ya maana ya elimu" kwa wanafunzi wote wenye ulemavu. Mahakama Kuu ya Marekani iliongeza kiwango cha FAPE katika *Endrew F.* ARCs zinahitajika na *Endrew F.* Kuunda IEP "zinazotekelezwa kwa njia inayofaa ili kumwezesha mtoto kufanya maendeleo yanayofaa kwa kuzingatia hali ya mtoto."

---

[1] *Bd. of Educ. of Hendrick Hudson Cent. Sch. Dist., Westchester Cty. v. Rowley*, 458 U.S. 176, 102 S. Ct. 3034 (1982).

[2] *Endrew F. ex rel. Joseph F. v. Douglas Cty. Sch. Dist. RE-1*, 137 S. Ct. 988, (2017) (akisisitiza kwamba ili kutimiza wajibu wake mkubwa chini ya IDEA, shule lazima itoe mpango wa elimu ya mtu binafsi (individual education plan (IEP)) unaoteklezwa kwa njia inayofaa ili kumwezesha mtoto kufanya maendeleo yanayofaa kwa kuzingatia hali ya mtoto.)

[3] *Deal v. Hamilton Cty. Bd. of Educ.*, 392 F.3d 840 (6th Cir. 2004)
(IDEA inahitaji IEP kutoa "mafao mazuri ya elimu" yaliyopimwa kuhusiana na uwezo wa mtoto husika.)

*Endrew F.* inarejelea *Rowley* ili kusaidia kuelezea jinsi ya kubaini wakati huduma za FAPE zimenyimwa. *Rowley* anajadili jaribio la sehemu mbili ambalo lazima litumike ili kubaini ikiwa huduma za FAPE zimenyimwa. Jaribio hili huzingatia maswali yafuatayo:

1. Je, wilaya imezingatia taratibu zilizowekwa katika IDEA?
2. Je, IEP ilitekelezwa kwa njia inayofaa, na ilimwezesha mwanafunzi kupata mafao ya elimu?

Swali la kwanza linauliza ikiwa kulikuwa na ukiukaji wowote wa utaratibu. Wafanyakazi wa wilaya na wazazi wanapaswa kukumbuka kwamba swali hili halikusudiwi kulaumu wilaya, ila linakusudiwa kuamua ni haki ambazo mwanafunzi hakupata.

*Mfano wowote wa kibinafsi* wa ukiukaji wa utaratibu lazima uchochee ARC kujibu kwamba wilaya haikufuata taratibu zilizowekwa katika IDEA.

Swali la pili ni tata zaidi. Ili kubaini ikiwa mwanafunzi alipata mafao ya elimu, ARC itahitaji kuangalia sheria nyingine za kesi. Katika kesi ya *Endrew F.*, Mahakama ya Kuu ya Marekani ilielezea, "Ili kutimiza wajibu wake mkubwa chini ya IDEA, shule lazima itoe IEP iliyotekelezwa ili kumwezesha mtoto kufanya maendeleo yanayofaa kwa kuzingatia hali ya mtoto." Ukaguzi wa data utasaidia ARC kufanya uamuzi huu.

***Ukaguzi wa Data***

Vyanzo vya data vinaweza kujumuisha, lakini sio tu, mambo yafuatayo:

- Maoni ya wazazi
- IEP ya sasa ya mwanafunzi
- Hati za elimu maalum na huduma zinazohusiana ambazo zilitolewa *na* hazikutolewa kwa mwanafunzi
- Alama za kabla ya, za wakati wa na baada ya NTI
- Sampuli za kabla ya, za wakati wa na baada ya NTI
- Kumbukumbu za mahudhurio ya NTI
- Taarifa kuhusu uwezo wa mwanafunzi wa kufikia intaneti, vifaa vya teknolojia ya moja kwa moja kama vile kompyuta kibao au kompyuta, kurekebishiwa hali na mazingira, teknolojia ya usaidizi na misaada na huduma za ziada
- Maendeleo ya kufikia malengo ya IEP ya kabla, ya wakati wa na ya baada ya NTI
- Tathmini, tathmini upya na tarehe za mwisho za kustahiki
- Uchunguzi usio rasmi/maelezo ya hadithi

ARC inapaswa pia kujadili ikiwa mwanafunzi alikuwa na fursa sawa ya kushiriki wakati wa NTI na vizuizi vyovyote ambavyo huenda vilimzuia mwanafunzi kujifunza kwa kutumia kwa mtaala wa jumla.

Zaidi ya hayo, ARC inapaswa kujadili jinsi wilaya ilivyopunguza vizuizi ili kukidhi mahitaji ya mwanafunzi huyo binafsi.

ARC inapaswa kujadili kiwango cha maendeleo ya mwanafunzi kabla ya NTI ya muda mrefu. ARC inaweza kuuliza maswali kama vile:

- Je, mwanafunzi aliweza kudumisha kiwango sawa cha maendeleo wakati wa NTI?
- Je, kulikuwa na tofauti kubwa katika maendeleo wakati mwanafunzi aliporudi kwenye mafundisho ya ana kwa ana?
- Je, kuna uwiano kati ya ongezeko la maendeleo na kizuizi cha kujifunza ambacho hakikuweza kupunguzwa kwa usalama wakati wa NTI?

Maswali ya ziada ambayo wanachama wa ARC wanaweza kuzingatia yanaweza kupatikana katika hati inayoambatana na inayoitwa *Maswali ya Kuongoza ARC kuhusu Elimu ya Mafunzo ya Ziada*.

**Kuamua Dakika za Huduma ya Elimu ya Mafunzo ya Ziada**

Kuna njia mbili za kuhesabu tuzo ya elimu ya mafunzo ya ziada. Njia moja ni njia ya dakika kwa dakika, au kiasi. Kwa njia hii, wilaya hutoa tarakimu kamili ya dakika za mafundisho ambazo mwanafunzi alikosa.

Njia nyingine ya kutoa elimu ya mafunzo ya ziada ni mbinu ya ubora. Katika mbinu ya ubora, uchambuzi wa kuamua ikiwa mwanafunzi anahitaji elimu ya mafunzo ya ziada, na hesabu ya kiasi gani, inaweza kuamualiwa na athari ya kupoteza faida ya elimu ambayo mwanafunzi alipata kulingana na hali yake ya kipekee. Hii inahitaji ARC ichunguze faida ambazo mwanafunzi angepokea ikiwa mwanafunzi angepewa FAPE.

Maamuzi kuhusu hitaji na aina za matoleo ya elimu ya mafunzo ya ziada lazima yafanywe kwa kuzingatia kila hali. Mahitaji ya elimu ya kila mwanafunzi ni ya kipekee, na kila mpango wa elimu unapaswa kuundwa kwa ajili ya mwanafunzi binafsi. ARC lazima iamue njia inayofaa zaidi kulingana na hali ya kibinafsi ya kila mwanafunzi. Mbinu zinazofanana au zisizobadilika za muundo wa elimu ya mafunzo ya ziada hazitafaa na hazitashughulikia mahitaji ya kibinafsi ya mwanafunzi.

**Mazingatio ya utaratibu wa ugavi na usafirishaji**

***Jinsi ya Kuandika Maamuzi ya Elimu ya Mafunzo ya Ziada***

Majadiliano kuhusu elimu ya mafunzo ya ziada lazima yaandikwe kikamilifu katika Muhtasari wa Mkutano wa ARC.

***Kupanga Mikutano ya ARC***

Wanafunzi wengine wenye ulemavu hupata changamoto kubwa zaidi wakianza kujifunza kwa NTI kuliko wengine. Wilaya zinaweza kupanga mikutano ya ARC haraka ili kujadili elimu ya mafunzo ya ziada kwa ajili ya wanafunzi waliopata changamoto kubwa zaidi wakati wa NTI.

Kwa wanafunzi waliopata changamoto chache wakati wa NTI, elimu ya mafunzo ya ziada inaweza kujadiliwa katika mikutano ya ukaguzi wa kila mwaka.

***Kupanga Huduma za Elimu ya Mafunzo ya Ziada***

Wakati wa kupanga vikao vya elimu ya mafunzo ya ziada, ARC lazima izingatie mambo kadhaa. Kwanza, wilaya lazima izingatie maudhui yatakayojadiliwa katika vikao. Ifuatayo, wilaya lazima iamue mtu akayesimamia vikao, mahali na ni mara ngapi vikao vitafanyika.

Maagizo yaliyoundwa kwa njia maalum lazima yatolewe na mwalimu wa elimu maalum. Huduma zinazohusiana lazima zitolewe na wafanyakazi wa shule walioidhinishwa ipasavyo, watoa huduma walio na kandarasi, au watoa huduma wa kibinafsi.

Vikao vya elimu ya mafunzo ya ziada lazima vitokee nje ya siku ya kawaida ya mafundisho. Huduma zinaweza kutolewa kabla ya au baada ya saa za kawaida za shule au wakati wa mapumziko ya shule.

Ufuatiliaji endelevu wa maendeleo unapaswa kukusanywa na kupitiawa na ARC ya mwanafunzi.

***Watoa Huduma wa Nje***

Wilaya zinaweza kufanya mkataba na watoa huduma wa nje ili kusaidia katika kutoa elimu ya mafunzo ya ziada; hata hivyo, hii haihitajiki. Kufanya mkataba na watoa huduma wa nje kunaweza kusaidia wilaya kupanga shughuli za wafanyakazi wakati wanapokabiliwa na wafanyakazi wachache.

Wakati wa kufanya mkataba na watoa huduma wa nje, wilaya zinapaswa kuzingatia kutengeneza michakato ya ndani ili kuhakikisha malipo ya huduma yanatolewa kwa wakati unaofaa.

***Usafiri***

Wilaya lazima itoe usafiri kwa wanafunzi wote wanaopata elimu ya mafunzo ya ziada.

Wilaya zinaweza kuwalipa wazazi gharama walizotumia wakati wazazi wako tayari na wanaweza kutoa huduma ya usafiri kwa watoto wao. Zinaweza kufanya hivi kwa kutumia kiasi cha malipo kwa kila maili.

Usafiri unaotolewa na mzazi unategemea makubaliano ya pande zote mbili yaani wazazi na wilaya [*Barua kwa Hamilton* (OSEP 1996); *Barua kwa Neveldine* (OSEP 1996)]. Ili wazazi warejeshewe gharama kwa ajili ya wanafunzi walio na IEP, lazima kuwe na idhini ya awali iliyoandikwa kutoka kwa wilaya na lazima izingatie IEP ya mwanafunzi.

Kiasi cha malipo kwa kila maili kinategemea miongozo ya Usimamizi wa Huduma za Jumla wa Marekani (General Services Administration (GSA)). Wilaya pia zinahitaji kufahamu kwamba wazazi wakikubali kusafirisha mwanafunzi mwenye ulemavu, wilaya lazima irejeshee wazazi gharama zao za usafiri kwa mujibu wa sera ya wilaya na makubaliano ya mkataba kama ilivyokubaliwa kati ya wilaya na mzazi. (*Mwongozo wa Usafiri Maalum huko Kentucky*, ukurasa wa 24).

***Mahudhurio***

Wilaya lazima ziandike waliohudhuria wakati wa vikao vya elimu ya mafunzo ya ziada. Kufuatilia mahudhurio kutasaidia katika kubaini ikiwa vikao vyote vimekamilika.

Wilaya ikighairi vikao vya elimu ya mafunzo ya ziada kwa sababu yoyote, vikao vilivyoghairiwa lazima vipangwe upya.

Mwanafunzi akikosa kuhudhuria vikao vya elimu ya mafunzo ya ziada vilivyopangwa, huenda ARC ikahitaji kupangwa ili kujadili sababu za kutokuwepo kwa mwanafunzi. ARC ikibaini kuwa kuna kizuizi kwa mahudhurio ya mwanafunzi, ARC inapaswa kujadili mpango wa elimu ya mafunzo ya ziada na kufanya marekebisho ili kuongeza mahudhurio.

***Mazingatio ya Kifedha***

Gharama haiwezi kuwa sababu ya kukataa kutoa huduma za elimu ya mafunzo ya ziada. Wilaya lazima zigharamie shughuli zote zinazohusiana na kutoa elimu ya mafunzo ya ziada.

Wilaya zinaweza kufikiria kuhifadhi sehemu ya ufadhili wa ESSER ili kulipia elimu ya mafunzo ya ziada. Isitoshe, wilaya zinapaswa kuzingatia kwa makini mahitaji ya Matengenezo ya Juhudi ya IDEA (Maintenance of Effort (MOE)), ambayo yamezungumziwa kwa kina zaidi katika *Mwongozo wa COVID-19 kwa Shule: Mfuko wa Usaidizi wa Dharura wa Shule za Msingi na Sekondari II (Elementary and Secondary School Emergency Relief Fund II (ESSER II))*.

***Idadi ya Wanafunzi***

Huduma za elimu ya mafunzo ya ziada zinaweza kutokea katika mazingira ya moja kwa moja au katika vikundi vidogo au madarasa. Idadi ya wanafunzi katika vikao vya elimu ya mafunzo ya ziada haipaswi kuzidi mahitaji ya idadi ya wanafunzi ya darasa la la kawaida. Huwezi kukubaliwa kukiuka kanuni ya idadi fulani ya wanafunzi kwa sababu tu darasa ni la elimu ya mafunzo ya ziada.

Kwa wanafunzi wa shule ya chekechea, ikiwa elimu ya mafinzo ya ziada hutolewa wakati wa kikao tofauti cha shule ya chekechea, kikao hakiwezi kuzidi wanafunzi 20.

***Fursa za Shule Nzima***

Shule na wilaya nyingi za Kentucky zimeunda fursa halisi, shirikishi, za elimu ya maffunzo ya ziada ili kusaidia wanafunzi wote waliopoteza fursa za kujifunza au kurudi nyuma kwa ujuzi wakati wa janga la COVID-19. Ni muhimu kukumbuka kuwa wanafunzi wenye ulemavu ni wanafunzi wa elimu ya jumla kwanza na wana haki ya fursa sawa. Wanafunzi wenye ulemavu pia wana haki ya kupata huduma za ziada zilizoelezewa katika IEP zao. Haitakuwa sahihi kutumia mpango wa kupata ujuzi unaotolewa kwa wanafunzi wote ili kutimiza dakika za elimu ya mafunzo ya ziada. Huduma za jumla zinazotolewa kwa wanafunzi wote haziwezi kuchukua nafasi ya huduma zinazohitajika za elimu ya mafunzo ya ziada zilizoamuliwa na ARC.

**Hati za Huduma za Elimu ya Mafunzo ya Ziada**

Wilaya zinapaswa kudumisha kumbukumbu ya kina ya huduma za elimu ya mafunzo ya ziada zinazotolewa pamoja na data ya ufuatiliaji wa maendeleo unaoendelea. Hii inapaswa kuhifadhiwa katika jalada la mchakato stahiki la mwanafunzi. Wilaya zinapaswa kuzingatia jinsi ya kufuatilia dakika za elimu ya mafunzo ya ziada kwa wanafunzi wote ndani ya wilaya.

Hati inayoambatana inayoitwa Kumbukumbu ya Elimu ya Mafunzo ya Ziada hutoa fomu ya mfano ya kuandika kuhusu elimu ya mafunzo ya ziada. Pia inaonyesha jinsi fomu iliyojazwa inavyoweza kufanana. Wilaya hazihitajiki kutumia kumbukumbu hii. Kumbukumbu zilizoundwa na wilaya lazima ziandike tarehe ya huduma, jina la mtoa huduma, mambo yaliyozungumziwa wakati wa kikao na idadi ya dakika zilizotolewa.

Walimu na watoa huduma wanapaswa kutaja mambo mahususi wanapojaza kumbukumbu za elimu ya mafunzo ya ziada. Kumbukumbu za kina huruhusu ARC kuchanganua vyema maendeleo ya mwanafunzi katika vikao vya elimu ya mafunzo ya ziada.

**Mambo Muhimu ya Kukumbuka:**

- Elimu ya mafunzo ya ziada ni suluhisho linalotolewa kwa mwanafunzi wakati amenyimwa huduma za FAPE. Imeundwa ili kumweka mwanafunzi mahali ambapo angekuwa kama hangekuwa amenyimwa FAPE.
- ARC lazima itengeneze mpango wa utekelezaji uliobinafsishwa wa huduma za elimu ya mafunzo ya ziada na kuandika maamuzi katika Muhtasari wa Mkutano wa ARC.
- Ufuatiliaji endelevu wa maendeleo lazima ukusanywe.
- Wilaya inawajibika kwa gharama zote zinazohusiana na kutoa huduma za elimu ya mafunzo ya ziada.
- Mwalimu wa elimu maalum lazima atoe mafundisho yaliyoundwa kwa njia maalum na mtoa huduma anayefaa lazima atoe huduma zinazohusiana.
- Wilaya lazima itoe au ilipie mwanafunzi usafiri.
- Kwa wanafunzi wa shule ya chekechea, ikiwa elimu ya mafinzo ya ziada hutolewa wakati wa kikao tofauti cha shule ya chekechea, kikao hakiwezi kuzidi wanafunzi 20.
- Huduma za jumla zinazotolewa kwa wanafunzi wote haziwezi kuchukua nafasi ya huduma zinazohitajika za elimu ya mafunzo ya ziada zilizoamuliwa na ARC.
- Wilaya zinapaswa kudumisha kumbukumbu ya kina ya huduma za elimu ya mafunzo ya ziada kama zinavyotolewa kwa mwanafunzi, ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa maendeleo unaoendelea. Hii inapaswa kuhifadhiwa katika jalada la mchakato stahiki la mwanafunzi.

# *Rasilimali za ARC*

# Maswali Yaliyopendekezwa ya Kuongoza ARC kuhusu Elimu ya Mafunzo ya Ziada

**Viwango vya Utendaji wa Kabla ya COVID wa Mwanafunzi:**

- Je, viwango vya sasa vya utendajiwa mwanafunzi vilikuwa vipi?
- Je, mwanafunzi alikuwa akifanya maendeleo yanayotarajiwa kwenye malengo ya IEP?
- Je, elimu gani maalum na huduma zinazohusiana zilibainishwa katika IEP ya mwanafunzi?

**Wakati wa NTI:**

- Je, mwanafunzi aliendelea kupokea huduma na usaidizi wa IEP vipi?
- Je, huduma na usaidizi gani wa IEP haukutolewa?
- Je, mwanafunzi alipitia vizuizi vya usawa na ufikiaji kama matokeo ya NTI? Je, wilaya ilishughulikiaje vizuizi hivyo? Je, kuna vizuizi vyovyote ambavyo havikuweza kuondolewa kwa sababu ya wasiwasi wa afya ya umma?
- Je, mahudhurio ya mwanafunzi na kiwango cha ushiriki kilikuwaje? Ikiwa hakikuwepo, je, jambo hii ilishughulikiwa vipi?
- Je, shule au wilaya ilibaini nyanja zozote mpya za wasiwasi kwa mwanafunzi? Ikiwa ndivyo, je, zilishughulikiwa vipi?
- Je, mwanafunzi aliitikia NTI vipi?
- Je, shule au wilaya ilishirikisha familia ya mwanafunzi vipi?

**Kurudi kwa Mafundisho ya Ana kwa Ana:**

- Je, viwango vya sasa vya mwanafunzi aliporudi kwenye mafundisho ya ana kwa ana vilikuwa gani?
- Je, mwanafunzi aliitikia vipi aliporudi kwa mafundisho ya ana kwa ana na/au mseto? Je, kulikuwa na tofauti gani zinazoonekana katika maendeleo kati ya NTI na mafundisho ya ana kwa ana?
- Je, ukaguzi wa data ulionyesha kwamba mwanafunzi anahitaji usaidizi na/au huduma za ziada?

**Kuamua Huduma za Fidia:**

- Je, kulikuwa na huduma ambazo mwanafunzi hakuweza kupewa kwa usalama wakati wa kujifunza akiwa mbali?
- Je, ukaguzi wa data unaonyesha kwamba mwanafunzi anahitaji huduma za ziada za IEP na/au usaidizi ili kufidia huduma ambazo hazikuweza kutolewa kwa usalama?
- Je, ARC itatumia mchakato gani kuamua elimu ya mafunzo ya ziada (ubora au kiasi)? Ikiwa ni ya ubora, ni itatekelezwa vipi?
- Ni maoni gani ya mzazi yalikusanywa kuhusiana na hitaji linalowezekana la mwanafunzi la huduma za fidia?

**Maswali ya utaratibu wa ugavi na usafirishaji:**

- Je, ratiba ya huduma za fidia itajumuisha nini? Je, nani atatoa huduma? Je, idadi ya marudio ya huduma ni gani? Je, eneo la huduma ni wapi?
- Je, maudhui gani yatafunzwa wakati wa elimu ya mafunzo ya ziada?
- Je, huduma ya safiri itatolewa vipi?
- Je, wilaya itaandika vipi wakati huduma zimetolewa?

## Mfano wa Kumbukumbu ya Elimu ya Mafunzo ya Ziada

Wilaya ya Shule ya Kujitegemea ya
Adams City Marcus DeWitt

| Tarehe | Jina la Mtoa huduma | Maudhui Yaliyofunzwa/Vidokezo | Idadi ya Dakika | Herufi za Kwanza za Majina ya Mtoa huduma |
|---|---|---|---|---|
| 3/5/21 | S. Ayad | Mafundisho ya moja kwa moja ya uundaji wa nambari | 27 | SA |
| 3/6/21 | S. Ayad | Hakuna kikao - mwalimu alikuwa mgonjwa | 0 | SA |
| 3/7/21 | S. Ayad | Mafundisho ya moja kwa moja ya kuzidisha takwimu za safu | 30 | SA |
| 3/8/21 | J. Hernandez | OT - Alishirikiana na mwanafunzi katika shughuli za kuimarisha mwendo wa misuli. | 25 | JH |
| 3/8/21 | J. Hernandez | OT - Alipitia mpango wa shughuli za kumtuliza mwanafunzi- -aliongeza shughuli za mwendo na kuzidisha shinikizo | 23 | JH |
| 3/10/21 | S. Ayad | Mafundisho ya moja kwa moja ya kujenga takwimu za safu | 29 | SA |
| 3/11/21 | M. Lanceta | Kuongea - mafundisho ya moja kwa moja ya kutamka konsonoti zenye /r/ | 30 | LL |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| **JUMLA YA DAKIKA KATIKA UKURASA HUU** | | | | **164** |
| **JUMLA YA KUONGEZEA** | | | | **564** |

# *Rasilimali kwa ajili ya Wazazi na Familia*

# Mwongozo wa Mzazi na Familia wa Mifano ya Kufundisha na Elimu ya Umma Inayofaa ya Bure (Appropriate Public Education (FAPE))

Wilaya za shule za eneo husika zinaweza kutumia mifano mbalimbali ya kufundisha:

| Ya Jadi | Ya Mseto | NTI | *Ya Kujisimamia |
|---|---|---|---|
| Jumatatu - Ijumaa, mafundisho ya ana kwa ana | mchanganyiko wa mafundisho ya ana kwa ana na yasiyo ya kawaida (Non-Traditional Instruction (NTI)) | Mafundisho Yasiyo ya Kawaida (Non-Traditional Instruction (NTI)) au mafundisho ya mtandaoni | kazi hutumwa nyumbani na mwanafunzi hukamilika kazi hiyo bila mwalimu kumsimamia sana |

** Mbinu ya Kufundisha ya Mwanfunzi Kujisimamia inaweza kutolewa na baadhi ya wilaya; hata hivyo elimu maalum haiwezi kutolewa bila mafundisho yaliyoundwa kwa njia maalum kutoka kwa mwalimu wa elimu maalum. Mafundisho yaliyoundwa kwa njia maalum yanahusisha kurekebisha maudhui, mbinu, au utoaji wa mafundisho kama inavyofaa, ili kushughulikia mahitaji ya kipekee ya mwanafunzi mwenye ulemavu na kuhakikisha kwamba mwanafunzi anaweza kujifunza kwa kutumia mtaala wa jumla. Kwa hivyo, bila utoaji wa SDI kwa mujibu wa IEP, mwanafunzi hunyimwa FAPE.*

Bila kujali eneo, Sheria ya Elimu ya Watu Wenye Ulemavu (Individuals with Disabilities Education Act (IDEA)) na kanuni zake za zinazotekelezwa zinaweka wazi kuwa wanafunzi wote wanaopata elimu maalum na huduma zinazohusiana wana haki ya kupata elimu ya umma inayofaa bure (free appropriate public education (FAPE)). **Elimu maalum inamaanisha mafundisho ambayo yameundwa mahususi kukidhi mahitaji ya kipekee ya mwanafunzi.** FAPE inahitaji elimu maalum na huduma zinazohusiana zitolewe bila gharama yoyote kwa wazazi. FAPE pia inajumuisha huduma zinazohusiana ambazo humsaidia mwanafunzi kufaidika na mpango wake wa elimu. Baadhi ya mifano ya huduma zinazohusiana ni pamoja na tiba ya kuongea, ya kimwili au ya shughuli za mwili.

Mpango wa Elimu ya Mtu Binafsi, unaojulikana kama IEP, ni mpango wa elimu unaoelezea uwezo, mahitaji, malengo ya mtoto wako na huduma zinazohitajika ili mtoto wako afanye maendeleo katika mtaala wa jumla. IEP ***sio*** mtaala wa mtoto wako. Watoto wote, ikiwemo watoto waliotambuliwa na ulemavu wana haki ya kujifunza kwa kutumia mtaala wa elimu ya jumla. IEP inabainisha kila kitu kinachopaswa kutekelezwa, kulingana na mahitaji ya kipekee ya mtoto wako, ili mtoto wako afanye maendeleo. Hapo chini kuna majibu ya maswali yanayoelezea mambo unayoweza kutarajia kuhusu utekelezaji wa IEP ya mtoto wako katika miundo mbalimbali ya utoaji wa wilaya. (*Mwongozo wa Wazazi wa Kentucky wa Elimu Maalum,* Machi 2019)

**Je, mtoto wangu atapata vipi elimu maalum (marekebisho ya maudhui na utoaji wa mafundisho)?**

| Ya Jadi | Ya Mseto | NTI |
|---|---|---|
| Elimu maalum na mafundisho ya moja kwa moja ya mwalimu wa elimu ya jumla darasani | Mwalimu(Walimu) wa elimu maalum hutoa mafundisho ya moja kwa moja darasani na mtandaoni au kwa simu | Mwalimu(Walimu) wa elimu maalum hutoa mafundisho ya moja kwa moja mtandaoni au kwa simu |

**Je, ninaweza kutarajia maendeleo ya mtoto wangu yafuatiliwe vipi?**

| Ya Jadi | Ya Mseto | NTI |
|---|---|---|
| Walimu wa elimu maalum na elimu ya jumla watakusanya data ya maendeleo kutoka kwa mafundisho darasani | Walimu wa elimu maalum na elimu ya jumla hukusanya data ya maendeleo inayoendelea kutoka kwa mafundisho darasani, mtandaoni, kwa simu, au kupitia kazi za karatasi zilizoundwa kwa ajili ya wanafunzi binafsi | Walimu wa elimu maalum na elimu ya jumla hukusanya data ya maendeleo inayoendelea kutoka kwa mafundisho mtandaoni, kwa simu, au kupitia kazi za karatasi zilizoundwa kwa ajili ya wanafunzi binafsi |

**Je, mtoto wangu atapokea vipi misaada na huduma za ziada ili kumsaidia kuendelea katika mtaala wa jumla?**

ARC lazima iamue misaada na huduma za ziada ambazo mwanafunzi atapewa. IEP itaelezea aina za misaada na huduma za ziada ambazo mwanafunzi anastahiki kupata na wakati ambapo huduma hizi zitatolewa. Baadhi ya mifano ya misaada na huduma za ziada ni pamoja na kutumia mfumo wa mawasiliano, kuchapisha maandishi makubwa, muda ulioongezwa wa kukamilisha kazi, vipangaji vya picha, ratiba za kuona, vipima muda vya kuona, mifumo ya kupanga, mapumziko ya kusogea sogea, usaidizi wa watu wazima, vifaa vya teknolojia ya usaidizi, n.k. (*Mwongozo wa Wazazi wa Kentucky wa Elimu Maalum,* Machi 2019)

| Ya Jadi | Ya Mseto | NTI |
|---|---|---|
| Mwanafunzi atapewa misaada na huduma za ziada kama inavyohitajika siku nzima ya masomo | Mwanafunzi atapewa misaada na huduma za ziada kama inavyohitajika siku nzima ya masomo | Mwanafunzi atapewa misaada na huduma za ziada kama inavyohitajika siku nzima ya masomo |

**Je, mtoto wangu atapokea vipi marekebisho ya kazi na majaribio (kwa mfano, msomaji, mwandishi, muda ulioongezwa)?**

| Ya Jadi | Ya Mseto | NTI |
|---|---|---|
| Marekebisho yatafanywa kama sehemu ya utaratibu wa kumfundisha mwanafunzi ndani ya darasa | Marekebisho yatafanywa kama sehemu ya utaratibu wa kumfundisha mwanafunzi ndani ya darasa la mtandaoni au la kawaida | Marekebisho yatafanywa kama sehemu ya utaratibu wa kumfundisha mwanafunzi ndani ya darasa la mtandaoni |

**Taarifa zaidi juu ya vipengele vya IEP ya mtoto wako:**

Mafundisho Yaliyoundwa kwa Njia Maalum

- Mambo ambayo mwalimu hufanya ili kufundisha, kutathmini na kumfundisha tena mtoto wako
- Yanajumuisha kurekebisha maudhui, mbinu na njia ya kufundisha
- Yameundwa na kutekelezwa kwa utaratibu ili kushughulikia mahitaji yaliyotathminiwa ya mtoto wako
- Yanahitajika ili mtoto wako afanye maendeleo ya kufikia malengo ya kila mwaka
- Yamepangwa, yameundwa na yalitekelezwa hapo awali na mwalimu wa elimu maalum na ni ya kipekee kwa mtoto wako

Misaada na Huduma za Ziada

- Mikakati, vifaa na huduma zinazohitajika ili kumsaidia mtoto wako kufikia malengo ya IEP
- Humsaidia mtoto wako kuhusika na kufanya maendeleo katika mtaala wa jumla
- Humpa mtoto wako fursa sawa ya kushiriki katika shughuli zisizo za masomo na za ziada

Kubainisha Marekebisho

- Huelezea mahitaji ya mtoto wako kwenye tathmini za jimbo na wilaya
- Huruhusu alama ya mtoto wako kuonyesha alichojifunza kwenye mtaala wa jumla
- Lazima yahusiane na ulemavu wa mtoto wako, na kuwe na uthibitisho wa tathmini
- Lazima yawe sehemu ya utaratibu wa kawaida wa kumfundisha mtoto wako
- Lazima yaamuliwe kila mwaka
- Utegemezi wa marekebisho unapaswa kupunguzwa kadiri ujuzi wa mtoto wako unavyoimarika

(*KARATASI YA UKWELI: IEP,* Taasisi ya Maendeleo ya Binadamu)

Rasilimali:

Mpango wa Ushiriki wa Wazazi

# Mwongozo wa Mzazi na Familia wa Elimu ya Mafunzo ya Ziada

*Mwongozo huu unakusudiwa kusaidia wazazi na familia kama wajumbe wa Kamati ya Uandikishaji na Ukaguzi (Admissions and Release Committee (ARC)) wakati wa majadiliano yanayojumuisha huduma za elimu ya mafunzo ya ziada.*

**Je, elimu ya mafunzo ya ziada ni nini?**

Wanafunzi wenye ulemavu chini ya Sheria ya Elimu ya Watu Wenye Ulemavu (Individuals with Disabilities Education Act (IDEA)) wana haki ya kupata elimu ya umma inayofaa bure (free appropriate public education (FAPE)). Wakati huduma za elimu maalum ndani ya Mpango wa Elimu Binafsi ya mwanafunzi (Individual Education Program (IEP)) hazitolewi, huduma za elimu ya mafunzo ya ziada zinaweza kuhitajika kama suluhisho la kutokuwa na uwezo au kukosa kutoa FAPE.

Elimu ya mafunzo ya ziada inapaswa kulenga kuwaweka wanafunzi wenye ulemavu katika nafasi ile ambayo wangechukua kama hakungekuwa na ukosefu wa uwezo au kushindwa kutoa FAPE.

**Je, wanafunzi wote watapewa huduma za elimu ya mafunzo ya ziada kwa sababu walipokea mafundisho kupitia mbinu ya NTI wakati wa Janga la COVID-19?**

Hapana. Huduma za elimu ya mafunzo ya ziada lazima ziamuliwe kulingana na kila hali.

**Je, mwanafunzi anaweza kupata elimu ya mafunzo ya ziada ikiwa ana umri wa zaidi ya miaka 21?**

Ndiyo. Ikiwa kutokuwa na uwezo au kushindwa kutoa FAPE kulitokea kabla ya mwanafunzi kufikia siku yake ya kuzaliwa ya 21 au kuhitimu, huduma za elimu ya mafunzo ya ziada zinaweza kuzingatiwa kama suluhisho na ARC (*Barua kwa Riffel*, Agosti 22, 2000).

**Je, ARC huzingatia taarifa gani wakati wa kuamua ikiwa mwanafunzi anahitaji huduma za elimu ya mafunzo ya ziada?**

ARC lazima iangalie mambo mengi wakati wa kuamua ikiwa kutokuwa na uwezo au kushindwa kutoa FAPE kumetokea. ARC inaweza kuzingatia, lakini sio:

- Maoni ya wazazi
- Huduma ambazo mwanafunzi binafsi alipokea au hakupokea
- Maendeleo au ukosefu wa maendeleo yanayotarajiwa ambayo mwanafunzi alifanya kwenye malengo ya IEP
- Uwezo wa mwanafunzi wa kupata huduma

**Je, kiasi cha huduma za elimu ya mafunzo ya ziada huhesabiwa vipi?**

Kuna njia mbili za kuhesabu tuzo ya elimu ya mafunzo ya ziada. Njia moja ni njia ya dakika kwa dakika, au kiasi. Kwa njia hii, wilaya hutoa tarakimu kamili ya dakika za mafundisho ambazo mwanafunzi alikosa.

Njia nyingine ya kutoa elimu ya mafunzo ya ziada ni mbinu ya ubora. Katika mbinu ya ubora, uchambuzi wa kuamua ikiwa mwanafunzi anahitaji elimu ya mafunzo ya ziada, na hesabu ya kiasi gani, inaweza kuamualiwa na athari ya kupoteza faida ya elimu ambayo mwanafunzi alipata kulingana na hali yake ya kipekee. Hii inahitaji ARC ichunguze faida ambazo mwanafunzi angepokea ikiwa mwanafunzi angepewa FAPE.

Maamuzi kuhusu hitaji na aina za matoleo ya elimu ya mafunzo ya ziada lazima yafanywe kwa kuzingatia kila hali. Mahitaji ya elimu ya kila mwanafunzi ni ya kipekee, na kila mpango wa elimu unapaswa kuundwa kwa ajili ya mwanafunzi binafsi. ARC lazima iamue njia inayofaa zaidi kulingana na hali ya kibinafsi ya kila mwanafunzi. Njia za kawaida sana za muundo wa elimu ya mafunzo ya ziada hazitafaa na hazitimizi mahitaji ya kibinafsi ya mwanafunzi.

**Je, huduma za elimu ya mafunzo ya ziada hutolewa vipi?**

Wakati wa kupanga huduma za elimu ya mafunzo ya ziada ambazo mwanafunzi anapata, ARC ya mwanafunzi, inayojumuisha wazazi wa mwanafunzi, lazima ifanye maamuzi kuhusu aina, eneo na kiasi cha huduma zitakazotolewa.

Huduma za elimu ya mafunzo ya ziada na usafiri wa kupokea huduma hizo hutolewa bila gharama kwa mzazi au familia.

**Je, huduma za elimu ya mafunzo ya ziada huwa sawa kwa wanafunzi wote?**

Hapana. Huduma za elimu ya mafunzo ya ziada zinapaswa kuamuliwa kulingana na hali husika. Wanafunzi wanaweza kupewa huduma kabla au baada ya shule, siku za wikendi au wakati wa msimu wa kiangazi, na pia watapokea huduma zilizobinafsishwa.

**Je, elimu ya mafunzo ya ziada na huduma za mwaka wa masomo zilizoongezwa ni sawa?**

Hapana. Huduma za elimu ya mafunzo ya ziada na huduma za mwaka wa masomo ulioongezwa (extended school year (ESY)) ni tofauti na wanafunzi wengine wanaweza kupokea zote mbili.

**Je, nani anaweza kutoa huduma za elimu ya mafunzo ya ziada?**

Wafanyakazi wa shule, mtoa huduma aliye na kandarasi, au mtoa huduma wa kibinafsi anaweza kutoa huduma za elimu za mafunzo ya ziada. ARC itaamua mtoa huduma anayefaa kulingana na hali husika.

Walimu wa elimu maalum lazima watoe mafundisho yaliyoundwa kwa njia maalum na mtoa huduma anayefaa lazima atoe huduma zinazohusiana (tiba ya kuongea, kimwili, n.k.).

**Je, naweza kufanya nini ikiwa sikubaliani na uamuzi uliofanywa na ARC?**

Kwa kawaida, wazazi na wilaya huwa na uhusiano mzuri na hushirikiana ili kufanya maamuzi. Hata hivyo, huenda kukawa na nyakati ambapo wazazi na wilaya hawakubaliani. Mara nyingi kutokubaliana huku kunaweza kutatuliwa kwa mkutano kati ya mzazi na mwakilishi wa shule. Kwa kushirikiana pamoja kwa njia isiyo rasmi, wazazi na wilaya wanaweza kudumisha uhusiano mzuri na kwa kawaida wanaweza kutatua mashaka yao haraka zaidi. Unaweza pia kuwasiliana na msimamizi mkuu ili kujadili wasiwasi wako.

Mkikosa kukubaliana, KDE inapendekeza kwamba wazazi wawasiliane kwanza na mkuu wa shule ya mwanafunzi au Mkurugenzi wa Elimu Maalum (Director of Special Education (DoSE)) katika wilaya ili kuhakikisha kuwa wanafahamu tatizo hilo. Kitabu chenye orodha ya majina kinapatikana mtandaoni ili kuwasaidia wazazi kuwasiliana na DoSE.

Njia hizi zikikosa kutatua matatizo, kuna machaguo mengine matatu ya utatuzi wa migogoro. Wahusika wanaweza kutatua mizozo ya IDEA kupitia upatanishi, malalamiko rasmi ya maandishi au usikilizaji wa kesi.

**Rasilimali za Ziada:**

*OSEP QA 20-01* SeptembA 28, 2020

Reid v. Dist. of Columbia, 43 IDELR 32 (D.C. Cir. 2005)

Endrew F. v. Douglas County[4]

*Mwongozo wa Covid-19 wa KDE wa 2.0*

*Ukurasa wa wavuti wa  Utatuzi wa Migogoro ya KDE*

[4]*Endrew F., By His Parents and Next Friends, Joseph F., et al. v. Douglas County School District RE-1*, 580 U.S. ___ (S. Ct., Machi 22, 2017) Wilaya lazima itoe IEP ambayo imehesabiwa kwa njia inayofaa ili kumwezesha mtoto kufanya maendeleo yanayofaa kwa kuzingatia hali ya mtoto.